

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 2 JANUARI 2019**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 2 Januari 2019**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote (Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa) yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam, zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 5 Desemba 2018. Kwa mwezi Januari 2019, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 141/lita (sawa na asilimia 5.80), Shilingi 212/lita (sawa na asilimia 8.69) na Shilingi 167/lita (sawa na asilimia 7.03), mtawalia. Vilevile, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 140.81/lita (sawa na asilimia 6.09), Shilingi 212.12/lita (sawa na asilimia 9.14) na Shilingi 166.02/lita (sawa na asilimia 7.40), mtawalia. Kwa kiasi kikubwa, ongezeko la bei za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa kwenye soko la ndani limetokana na kushuka kwa bei za mafuta hayo katika soko la dunia kama inavyoonekana katika Jedwali C.
- (b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote (Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa) yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Tanga zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 5 Desemba 2018. Kwa mwezi Januari 2019, bei za rejareja za Petroli na Dizeli kwa **Mikoa ya Kaskazini** zimepungua kwa Shilingi 237/lita (sawa na asilimia 9.73) na Shilingi 138/lita (sawa na asilimia 5.80), mtawalia, wakati bei za Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 4/lita (sawa na asilimia 0.19). Aidha, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimepungua kwa Shilingi 236.31/lita (sawa na asilimia 10.23) na Shilingi 137.56/lita (sawa na asilimia 6.10), mtawalia, wakati bei za jumla za Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 4.19/lita (sawa na asilimia 0.20). Mabadiliko ya bei za mafuta kwa Mikoa ya Kaskazini yanatokana na kushuka kwa bei za mafuta hayo katika soko la dunia, kuongezeka kwa gharama za uagizaji na usafirishaji wa mafuta hayo (*BPS Premium*), na kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani, fedha inayotumika kununua mafuta.
- (c) Hakuna shehena ya mafuta iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Tanga katika mwezi wa Desemba 2018. Kwakuwa hakuna Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa katika maghala ya mafuta mkoani Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zinatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika.
- (d) Ni vema ikafahamika kuwa, tofauti ya mabadiliko ya bei za mafuta kati ya mafuta yaliyopokelewa nchini kupitia bandari za Dar es Salaam an Tanga inatokana na kuwa ulinganifu wa mabadiliko ya bei za mafuta yaliyopokelewa Dar es Salaam ni kati ya bei za mafuta katika soko la dunia kwa mwezi Novemba 2018 na Oktoba 2018 wakati; ulinganifu wa bei za Tanga ni kati ya bei za mafuta katika soko la dunia kwa mwezi Novemba 2018 na Septemba 2018

kwakuwa shehena ya mwisho kupokelewa katika bandari ya Tanga ilikuwa ni mwezi Oktoba 2018 ambayo ilinunuliwa kwa bei ya soko la dunia ya mwezi Septemba 2018.

- (e) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba **\*152\*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (f) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (g) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 163 la mwezi Aprili 2018 na Gazeti la Serikali Na. 269 la mwezi Juni 2018.****
- (h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahishisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mafuta ya petroli.

### JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
<b>Dar es Salaam</b>	<b>2,295</b>	<b>2,224</b>	<b>2,202</b>
<b>Arusha</b>	<b>2,255</b>	<b>2,299</b>	<b>2,286</b>
Arumeru (Usa West)	2,255	2,299	2,286
Karatu	2,273	2,318	2,304
Longido	2,266	2,310	2,297
Monduli	2,260	2,305	2,291
Monduli-Makuyuni	2,265	2,309	2,296
Ngorongoro (Loliondo)	2,340	2,384	2,371
<b>Pwani (Kibaha)</b>	<b>2,300</b>	<b>2,228</b>	<b>2,206</b>

Bagamoyo	2,306	2,235	2,213
Chalinze Junction	2,309	2,238	2,216
Chalinze (Msata)	2,313	2,242	2,220
Kibiti	2,316	2,244	2,222
Kisarawe	2,302	2,231	2,209
Mkuranga	2,305	2,234	2,211
Rufiji	2,323	2,252	2,229
<b>Dodoma</b>	<b>2,354</b>	<b>2,283</b>	<b>2,260</b>
Bahi	2,361	2,290	2,268
Chamwino	2,349	2,278	2,256
Chemba	2,380	2,309	2,287
Kondoa	2,387	2,316	2,293
Kongwa	2,351	2,280	2,258
Mpwapwa	2,355	2,284	2,262
Mtera (Makatopora)	2,373	2,302	2,279
<b>Geita</b>	<b>2,461</b>	<b>2,389</b>	<b>2,367</b>
Bukombe	2,450	2,378	2,356
Chato	2,482	2,410	2,388
Mbogwe	2,499	2,427	2,405
Nyang'hwale	2,476	2,404	2,382
<b>Iringa</b>	<b>2,359</b>	<b>2,288</b>	<b>2,266</b>
Ismani	2,364	2,293	2,271
Kilolo	2,364	2,292	2,270
Mufindi (Mafinga)	2,369	2,298	2,276
<b>Kagera (Bukoba)</b>	<b>2,511</b>	<b>2,439</b>	<b>2,417</b>
Biharamulo	2,485	2,414	2,392
Karagwe (Kayanga)	2,527	2,456	2,434
Kyerwa (Ruberwa)	2,533	2,462	2,439
Muleba	2,511	2,439	2,417
Ngara	2,498	2,427	2,405
Misenyi	2,519	2,448	2,426
<b>Katavi (Mpanda)</b>	<b>2,503</b>	<b>2,432</b>	<b>2,410</b>
Mlele (Inyonga)	2,485	2,414	2,392
Mpimbwe (Majimoto)	2,495	2,424	2,402
<b>Kigoma</b>	<b>2,527</b>	<b>2,455</b>	<b>2,433</b>
Uvinza (Lugufu)	2,539	2,468	2,445
Buhigwe	2,516	2,445	2,422
Kakonko	2,484	2,412	2,390
Kasulu	2,513	2,441	2,419
Kibondo	2,491	2,420	2,397
<b>Kilimanjaro (Moshi)</b>	<b>2,245</b>	<b>2,289</b>	<b>2,276</b>
Hai (Bomang'ombe)	2,248	2,292	2,279
Mwanga	2,238	2,282	2,269
Rombo (Mkuu)	2,261	2,306	2,292
Same	2,231	2,275	2,262
Siha (Sanya Juu)	2,251	2,295	2,282
<b>Lindi</b>	<b>2,354</b>	<b>2,283</b>	<b>2,261</b>
Lindi-Mtama	2,372	2,301	2,279

Kilwa Masoko	2,329	2,258	2,236
Liwale	2,375	2,304	2,282
Nachingwea	2,383	2,312	2,290
Ruangwa	2,385	2,314	2,292
<b>Manyara (Babati)</b>	<b>2,289</b>	<b>2,333</b>	<b>2,320</b>
Hanang (Katesh)	2,300	2,344	2,331
Kiteto (Kibaya)	2,304	2,349	2,335
Mbulu	2,302	2,346	2,333
Simanjiro (Orkasumet)	2,321	2,365	2,352
<b>Mara (Musoma)</b>	<b>2,474</b>	<b>2,403</b>	<b>2,380</b>
Musoma Vijijini (Busekela)	2,514	2,443	2,421
Rorya (Ingirijuu)	2,483	2,411	2,389
Rorya (Shirati)	2,517	2,446	2,424
Bunda	2,465	2,394	2,371
Butiama	2,471	2,399	2,377
Serengeti (Mugumu)	2,519	2,448	2,426
Tarime	2,485	2,414	2,391
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,489	2,418	2,396
<b>Mbeya</b>	<b>2,402</b>	<b>2,331</b>	<b>2,309</b>
Chunya	2,412	2,341	2,318
Chunya (Makongolosi)	2,426	2,355	2,333
Kyela	2,418	2,347	2,325
Mbarali (Rujewa)	2,386	2,315	2,293
Rungwe (Tukuyu)	2,411	2,340	2,318
<b>Morogoro</b>	<b>2,320</b>	<b>2,249</b>	<b>2,227</b>
Mikumi	2,336	2,265	2,242
Kilombero (Ifakara)	2,358	2,287	2,265
Kilombero (Mlimba)	2,380	2,309	2,287
Kilombero (Mngeta)	2,370	2,298	2,276
Ulanga (Mahenge)	2,369	2,297	2,275
Malinyi	2,379	2,308	2,285
Kilosa	2,339	2,267	2,245
Gairo	2,339	2,267	2,245
Mvomero (Wami Sokoine)	2,331	2,259	2,237
Mvomero (Sanga Sanga)	2,320	2,249	2,227
Turiani	2,345	2,274	2,252
<b>Mtwara</b>	<b>2,368</b>	<b>2,296</b>	<b>2,274</b>
Nanyumbu (Mangaka)	2,416	2,345	2,323
Masasi	2,393	2,322	2,300
Newala	2,400	2,328	2,306
Tandahimba	2,393	2,322	2,299
Nanyamba	2,393	2,322	2,299
<b>Mwanza</b>	<b>2,445</b>	<b>2,374</b>	<b>2,352</b>
Kwimba	2,463	2,392	2,370
Magu	2,453	2,382	2,360
Misungwi	2,440	2,368	2,346
Sengerema	2,478	2,407	2,384
Ukerewe	2,505	2,434	2,411

<b>Njombe</b>	<b>2,388</b>	<b>2,316</b>	<b>2,294</b>
Njombe (Kidegembye)	2,408	2,337	2,315
Ludewa	2,425	2,354	2,332
Makambako	2,380	2,309	2,286
Makete	2,418	2,347	2,325
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,385	2,314	2,292
<b>Rukwa (Sumbawanga)</b>	<b>2,468</b>	<b>2,397</b>	<b>2,375</b>
Sumbawanga Rural (Mtowisa)	2,468	2,397	2,375
Kalambo (Matai)	2,475	2,404	2,382
Nkasi (Namanyele)	2,482	2,410	2,388
<b>Ruvuma (Songea)</b>	<b>2,419</b>	<b>2,347</b>	<b>2,325</b>
Mbinga	2,452	2,381	2,359
Namtumbo	2,448	2,377	2,355
Nyasa (Mbamba Bay)	2,462	2,391	2,369
Tunduru	2,478	2,406	2,384
<b>Shinyanga</b>	<b>2,424</b>	<b>2,353</b>	<b>2,331</b>
Kahama	2,438	2,367	2,344
Kishapu	2,453	2,381	2,359
Ushetu (Nyamilangano)	2,455	2,384	2,362
Simiyu (Bariadi)	2,466	2,394	2,372
Busega (Nyashimo)	2,459	2,387	2,365
Itilima (Lagangabilili)	2,469	2,397	2,375
Maswa	2,457	2,386	2,364
Meatu (Mwanhuzi)	2,464	2,393	2,371
<b>Singida</b>	<b>2,386</b>	<b>2,315</b>	<b>2,292</b>
Iramba	2,398	2,327	2,305
Manyoni	2,370	2,299	2,277
Ikungi	2,381	2,310	2,288
Mkalama (Nduguti)	2,410	2,339	2,317
<b>Songwe (Vwawa)</b>	<b>2,411</b>	<b>2,340</b>	<b>2,318</b>
Songwe (Mkwajuni)	2,418	2,347	2,325
Ileje	2,415	2,344	2,322
Momba (Chitete)	2,421	2,349	2,327
Tunduma	2,416	2,344	2,322
<b>Tabora</b>	<b>2,449</b>	<b>2,378</b>	<b>2,356</b>
Igunga	2,403	2,332	2,310
Kaliua	2,468	2,397	2,375
Ulyankulu	2,463	2,391	2,369
Nzega	2,414	2,343	2,320
Sikonge	2,461	2,390	2,368
Urambo	2,463	2,391	2,369
Uyui	2,450	2,379	2,357
<b>Tanga</b>	<b>2,198</b>	<b>2,243</b>	<b>2,229</b>
Handeni	2,219	2,263	2,250
Kilindi	2,234	2,278	2,265
Korogwe	2,210	2,255	2,241
Lushoto	2,220	2,264	2,251
Mkinga (Maramba)	2,205	2,250	2,236

Muheza	2,203	2,247	2,234
Pangani	2,205	2,249	2,236

### JEDWALI B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla – DSM	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,170.88	2,099.55	2,078.05

  

Bei za Jumla – TANGA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,074.48	2,118.21	2,105.56

  

Bei za Jumla - MTWARA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	----	----	-----

### JEDWALI C: SABABU ZA MABADILIKO YA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

#### BANDARI YA DAR ES SALAAM

	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Bei za mafuta katika soko la dunia	Punguzo la Dola 71.898/Tani	Punguzo la Dola 115.922/Tani	Punguzo la Dola 112.451/Tani
Gharama za usafirishaji wa mafuta ( <i>BPS premiums</i> )	Punguzo la Dola 3.050/Tani	Ongezeko la Dola 1.684/Tani	Ongezeko la Dola 1.800/Tani

#### BANDARI YA TANGA

	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Bei za mafuta katika soko la dunia	Punguzo la Dola 151.856/Tani	Punguzo la Dola 90.312/Tani	Punguzo la Dola 28.605/Tani
Gharama za usafirishaji wa mafuta ( <i>BPS premiums</i> )	Ongezeko la Dola 12.98/Tani	Ongezeko la Dola 10.72/Tani	Ongezeko la Dola 26.00/Tani

### JEDWALI D: BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA ZILIZOTUMIKA KUKOKOTOA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

	Bandari	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
<b>Mafuta yalipokelewa mwezi wa:</b>	<b>DSM</b>	Desemba 2018	Desemba 2018	Desemba 2018
	<b>Tanga</b>	Desemba 2018	Desemba 2018	Desemba 2018
	<b>Mtwara</b>	--	--	--
<b>Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa mwezi:</b>	<b>DSM</b>	Novemba 2018	Novemba 2018	Novemba 2018
	<b>Tanga</b>	Novemba 2018	Novemba 2018	Novemba 2018
	<b>Mtwara</b>	--	--	--

<b>Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa miezi inayoonekana hapo juu inalinganishwa na wastani wa bei za mwezi:</b>	<b>DSM</b>	Oktoba 2018	Oktoba 2018	Oktoba 2018
	<b>Tanga</b>	Septemba 2018	Septemba 2018	Julai 2018
	<b>Mtwara</b>	--	--	--

**Nzinyangwa E. Mchany**  
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**  
**EWURA**